TAMKO



Tamko la Afrika

kuhusu

Injili ya Ufanisi

na

Theolojia ya Neno la Imani

THE EKKLESIA AFRIKA

Tamko la Afrika

kuhusu

Injili ya Ufanisi

na

Theolojia ya Neno la Imani

THE EKKLESIA AFRIKA · NAIROBI · 2025

Tamko la Afrika kuhusu Injili ya Ufanisi na Theolojia ya Neno la Imani

Hakimiliki © 2025 na North Point Baptist Church (Kenya) na imeidhinishwa chini ya leseni ya CC BY-ND 4.0. Kuona nakala ya leseni hii tafadhali tembelea tovuti https://creativecommons.org/lecenses/by-nd/4.0/

Kimechapishwa na The Ekklesia Afrika Ltd

P. O. Box 52861-00100

Nairobi, Kenya

The Ekklesia Afrika Ltd ni shirika lililosajiliwa nchini Kenya.

Muundo wa jalada: Otieno Obunga

Imetafsiriwa na Cornerstone Baptist Church, Nairobi, kwa ushirikiano na Mchungaji Richard Elia (Tanzania)

Kimechapishwa mara ya kwanza 2025

Kimechapishwa Kenya: Jalada ngumu ISBN: 978-9914-759-13-6

Yaliyomo

Dibaji	5
Vifungu Vya Tamko	7
Waliotia Sahihi Mwanzoni	21
Jinsi Unavyoweza Kushiriki	25
Marejeo yanayopendekezwa	27

Dibaji

Katika kila kizazi, kanisa la Yesu Kristo hukabiliana na hatari nyingi. Baadhi yao huibuka kutoka nje. (MATENDO YA MITUME 20:29). Hata hivyo, lile ambalo ni hatari zaidi ni lile ambalo huibuka kutoka ndani. (MATENDO YA MITUME 20:30). Waandishi wa Biblia walikuwa na busara kwa hatari hizi walipoonya kuhusu mafundisho ya uongo na hatari za walimu wa uongo. Maonyo mengine ni mwito kwa kanisa kuwa macho na kuchambua kwa makini ili kulinda imani ya thamani iliyokabidhiwa watakatifu wote mara moja (YUDA 3). Na makanisa mengine ya kimitume yamejikita sana kuhubiri injili nyingine ambayo imetangazwa kuwa chini ya laana (WAGALATIA 1:8).

Katika wakati wetu wa karne ya ishirini na moja, kanisa bado linakabiliana kutokana na hatari nyingi za mafundisho potofu kama iliyotahadharishwa na mitume katika Agano Jipya. Mwito wa kuchambua na kuwa macho hutumika hata kwetu hivi leo jinsi ilivyokuwa kwao wakati ule. Hatari kuu siku hizi ni mafundisho yanayojulikana kama *Injili ya Ufanisi na Neno la Theolojia la Imani*. Mafundisho haya yanashikilia na kusisitiza mfumo wa mafundisho yanayounga mkono na kushikilia kwamba, kimsingi, afya na mali imehakikishiwa wakristo kama mojawapo ya matokeo ya kazi ya upatanisho ya Mwana wa Mungu msalabani. Hizi baraka za ufanisi lazima zifike kikomo kupitia mazoezi ya imani yanayojumuisha utoaji wa kifedha hadi kukiri ukweli wa neno la Mungu.

Mtazamo wa juu wa makanisa ya mahali fulani katika bara la Afrika inaonyesha kwamba, haya mafundisho yameingia katika makanisa mengi na kuwa ndiyo mafundisho yao halisi. Hata makanisa ambayo yanajivunia **tamko** thabiti la imani, yameingiliwa na haya mafundisho ya afya na mali ili kuharibu **tamko** lao la msingi wa imani. Inakuwa vigumu mno kuamini kwamba kwa sababu tu kusanyiko linabeba jina "Presbyterian," hivyo litashikilia mafundisho yaliyowekwa katika maungamo ya Westminster. Si kwamba tu kusanyiko linabeba jina "Anglican," haimaanishi kwamba linafuata Makala Thelathini na Tisa za imani. Si kwamba tu kusanyiko linabeba jina "Baptist," haimaanishi linashikilia **tamko** la maungamo ya imani ya London ya mwaka wa 1689, maungamo mapya ya (New Hampshire) na mengineyo.

Hivyo basi, kuna haja ya kuwa na tamko ambalo libainisha wazi mipaka kati ya wale wanaoshikilia na wale wasiounga mkono injili ya ufanisi na Neno la Theolojia la Imani. Kinachofuatia sasa ni mtiririko wa makubalio na kukana hadi mwisho. Lengo letu si kuleta mgawanyiko bali kusaidia kufafanua wazi msimamo wa makusanyiko na madhehebu tofauti kuhusu fundisho hili lenye hatari. Tumaini letu ni kwamba wengi watakubali **tamko** hili na kwamba watajitolea kulinda watu wa Mungu dhidi ya janga hili.

Kwa Utatu wa Utukufu wa Mungu pekee!

Vifungu vya Tamko

Kifungu cha 1

Tunakubaliana na kukiri kwamba Baba yetu wa mbinguni ni mwema, na hupendezwa kuwapa watoto wake zawadi njema. Tunakubaliana na kukiri kwamba zawadi zote njema kama afya, na mali hutoka kwa Mungu pasipo nia yoyote ya siri. Tunakubaliana na kukiri kwamba hizo zawadi hutolewa na Mungu kwetu kwa kadri ya neema yake bure. Tunakubaliana na kukiri kwamba ametupatia hizi zawadi ili tufurahie na tuzipokee kwa njia ya shukrani na unyenyekevu.

Tunakana kwamba Baba yetu wa mbinguni amehakikishia baraka zote za afya na mali kwa watoto wake kwa kuwa wameweka imani kwake. Tunakana kwamba afya na mali katika maisha haya ndiyo alama za ushirika wetu na yeye na kwamba kukosa hizo baraka inaashiria alama ya kukosa kunyakuwa kikamilifu mpango na nia yake ya maisha yetu duniani.

(1 Samweli 2:7; Mathayo 7:11; 1 Timotheo 6:17; Yakobo 1:17)

Kifungu cha 2

Tunakubaliana na kukiri kwamba kifo cha Yesu msalabani imetuhakikishia baraka zote zinazohusiana na wokovu wetu hapa duniani na hata milele. Tunakubaliana na kukiri kwamba muundo wa msamaha wetu ni kwamba katika toba na imani tumeunganishwa na Kristo na tunafurahia baraka za kuwekwa huru, kutakaswa na kutukuzwa baadaye. Tunakubaliana na kukiri kwamba wokovu wa miili yetu na kupokea afya kamilifu na mali ni sehemu ya wokovu ambayo itakuja kwa wakati wa kutukuzwa.

Tunakana kwamba kazi ya msamaha wa dhambi ya Yesu Kristo msalabani, inatusimamia baraka zote za afya na mali hapa duniani. Tunaendelea kukana kwamba ukamilifu uliokusudiwa katika wokovu uliopatikana kupitia msalaba utafurahiwa kikamilifu na watakatifu katika maisha haya kwa tofauti ndogo sana kati ya yale yanayohusiana na wakati huu na yale yatakayokuja katika nyakati ya utukufu.

(Warumi 4:25, 8:23; 2 Wakorintho 5:21; Waefeso 1:1-11; Tito 2:11-14; Waebrania 10:14; 1 Petro 2:24-25; Ufunuo 21:1-7)

Kifungu cha 3

Tunakubaliana na kukiri kwamba maana iliyokusudiwa na Roho Mtakatifu katika kifungu chochote cha Maandiko Matakatifu inaweza kufahamika kwa kutumia njia za kawaida za uchambuzi wa lugha ya Maandiko yanayozingatiwa. Tunaendelea kukubaliana na kukiri kwamba kila andiko la Biblia lazima izingatie muktadha halisi iliyotolewa au kuwekwa kulingana na muktadha wa kawaida na theolojia ya kimaandiko. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba tafsiri zozote za kimaandiko lazima ziwe sahihi kwa kiwango fulani namna ambavyo kanisa la kweli limesimama kwa kipindi chote cha historia.

Tunakana kwamba maandiko itafsiriwe kwa njia isiyo na mpangilio kulingana na maono binafsi au kwa njia ya mafumbo ya moja kwa moja. Tunakana kwamba kuna ufunuo fiche ndani ya maandiko ambayo waliotiwa mafuta tu ndiyo wanaweza kujua na kufunza. Tunakana kwamba matumizi ya akili yetu katika kuelewa maandiko hufanya kuwa bure kazi ya Roho Mtakatifu katika kutoa mwangaza wa kiroho.

(Luka 24:26–27, 44–47; Yohana 5:39–40; Warumi 15:4; 2 Timotheo 3:16–17; 2 Petro 1:20–21, 3:16–17)

Kifungu cha 4

Tunakubaliana na kukiri kwamba agano la Mungu na wana wa Israeli kwa maandiko ni tafakari ya hakika katika historia ya ukombozi. Tunakubaliana na kukiri katika agano hili la kale Mungu alihakikishia ufanisi wa mali kwa nchi ya Israeli kama ishara ya wema wake na upendo wake kwao. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba kwa sharti la kutii agano la kale, wana wa waisraeli walikuwa na haki halali ya kudai baraka za mali kutoka kwa mwenyezi Mungu kama ilivyo katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 28. Hata hivyo, Israeli, haikupata hizo baraka milele.

Tunakana kwamba hivi leo Wakristo wako katika uhusiano sawa na mwenyezi Mungu kama ilivyo kwa wana wa Israeli chini ya agano la kale. Kwa hivyo Tunakana kwamba hivi leo wakristo wana haki ya kudai baraka za mali kama ilivyoahidiwa katika agano la kale.

(Mwanzo 12:2–3; Kutoka 19:4–6; Mambo ya Walawi 26:3–13; Kumbukumbu la Torati 7:13–14, 28:1–2; Malaki 3:10–12)

Kifungu Cha 5

Tunakubaliana na kukiri kwamba chini ya mpangilio wa mpango wa Mungu, Mwisraeli aliyeshindwa kwa uovu mkubwa kutii masharti ya agano alistahili laana ya Mungu. Tunakubaliana na kukiri kwamba, matokeo ya kuvunja agano mara nyingine ingeweza hata kufuata vizazi vijavyo. Tunakubaliana na kukiri zaidi kwamba, Mungu mwenyewe ndiye aliye na haki ya kuadhibu uovu hadi kizazi cha nne, jambo ambalo lilihusisha ujuzi wake wa hatia yao mbele yake. Tunakubaliana na kukiri kwamba hali hiyo ilifika kileleni wakati Yesu alipochukuliwa kuwa na laana na hivyo akafa kwa ajili ya watu wake.

Tunakana kwamba wakristo wa kweli leo wanaweza kuwa chini ya laana yoyote, iwe ya vizazi au vinginevyo, kwa sababu ya dhambi zao au kwa sababu ya Babu zao wasioamini. Tunakana kwamba wakristo wanahitaji kufanya uchunguzi wa kina kuhusu historia ya familia yao na hivyo kutafuta ukombozi wa kipekee kutoka kwa kile wanakiita "minyororo ya vizazi," zaidi ya ukombozi unaopatikana mtu anapookolewa katika Kristo. Tunakana zaidi kwamba ukombozi huo maalum hupatikana kwa kutembelea maeneo maalum ya maombi, kushauriana na kupakwa mafuta maalum au kwa kutoa sadaka ya kifedha.

(Kutoka 20:5; Mambo ya Malawi 26:14-39; Kumbukumbu la Torati 11:26-28, 30:15-20; Yeremia 32:18-19; Wagalatia 3:13)

Kifungu Cha 6

Tunakubaliana na kukiri kwamba katika agano la kale, Mungu alijifunua kwa watu kupitia, madhahabu, hema ya kukutania, na hekalu. Tunakubaliana na kukiri kwamba maeneo haya yalikuwa mahali ambapo Mungu na mwanadamu walikutana. Hivyo, Tunakubaliana na kukiri kwamba madhahabu, hema ya kukutania na hekalu zilikuwa halali katika ibada ya watu wa Mungu. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba hayo yote yalitimia katika Kristo ambaye ni ufunuo wa mwisho wa Mungu na mahali pa kukutana kati ya Mungu na wanadamu. Tunakubaliana na kukiri kwamba baada ya Mungu, hakuna mahali duniani penye umuhimu wa kipekee wa kiroho kama njia ya kupata baraka za Mungu.

Tunakana kwamba majengo ya makanisa ya leo yanapaswa kuwa na madhabahu zinazotumika kama njia ya kuunganishwa na mbingu. Pia Tunakana kwamba wakristo wanapaswa “kuinua” madhabahu zinazoonekana au zisizoonekana ili kupata mamlaka ya kiroho juu ya eneo fulani. Tunakana kwamba ukombozi maalumu unahitajika ili kubomoa madhabahu zisizoonekana ili kuondoa uovu wa kiroho katika familia, makanisa, miji au mataifa.

(Mwanzo 13:4; Kutoka 25:8-9; Yohana 2:19-22, 4:21-23; Waebrania 8:1-2, 9:11-12, 24; 10:19-22)

Kifungu Cha 7

Tunakubaliana na kukiri kwamba mateso ya aina mbalimbali ni sehemu ya kawaida ya maisha katika ulimwengu huu ulioanguka. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba Mungu hupanga mateso kwa watu wake kwa makusudi mema ya upendo na ya hekima. Tunakubaliana na kukiri kwamba mateso hayapaswi kuonekana kama jambo la ajabu kwa wakristo. Hata hivyo, Tunakubaliana na kukiri kwamba sehemu ya tumaini la kikristo ni kuondolewa kwa mateso katika utukufu ujao. Tunakubaliana kukiri kwamba ingawa wakristo wanapaswa kuvumilia mateso kwa uvumilivu na hata kufurahi ndani yake, lakini hawapaswi kuyatafuta.

Tunakana kwamba mateso huja kwa sababu ya udhaifu wa imani yetu. Tunakana kwamba mateso hutokea kinyume na mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu. Pia Tunakana kwamba kuwepo kwa mateso katika maisha yetu kunahitaji ukombozi maalum unaohusisha kutoa fedha kwa "watumishi wa Mungu," kwa matamko ya unabii.

(Yohana 16:33; Matendo ya Mitume 14:22; Warumi 5:3-5, 8:17-18; 2 Wakorintho 1:3-5; Wafilipi 1:29, 3:10; 2 Timotheo 3:12; Yakoko 1:2; 1 Petro 4:12-19)

Kifungu Cha 8

Tunakubaliana na kukiri kwamba utoaji wa kifedha kwa kanisa la mahali ni nidhamu ya kiroho yenye manufaa. Tunakubaliana na kukiri kwamba wakristo wameitwa kuwa wakarimu, waaminifu na wa kujitoa katika kutoa kwao kifedha. Tunakubaliana na kukiri kwamba kwa kufanya hivyo wanajiwekea hazina mbinguni ambako nondo na kutu haviwezi kuharibu wala wezi kuiba. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba ni heri kutoa kuliko kupokea, na kwamba katika fursa ya kutoa kuna matunda na baraka kutoka kwa Mungu.

Tunakana kwamba utoaji wa kifedha umewekwa na Mungu kama njia ya kupata au kufikia baraka afya na utajiri. Tunakana kwamba wakristo wanaweza kununua miujiza kutoka kwa Mungu au kwamba Mungu huwanyima neema zake kwa wale wasiotoa kiasi fulani cha fedha. Pia Tunakana kwamba kushindwa kutoa asilimia 10 ya mapato kunaleta laana ya Mungu juu ya Mkristo kwa njia ya matatizo kama vile magonjwa na hasara.

(Matendo ya Mitume 20:35; 2 Wakorintho 8:1-5, 9:6-11; Waefeso 4:2; 1 Timotheo 6:6-10, 17-19; Waebrania 13:16)

Kifungu Cha 9

Tunakubaliana na kukiri kwamba maneno yetu yanaweza kuleta madhara makubwa au msaada kwa wengine. Kwa maana hiyo, Tunakubaliana na kukiri kwamba uzima na mauti, kwa mfano wa mithali, viko katika uwezo wa ulimi. Hivyo, maneno yana nguvu fulani ya ushawishi. Kwa hiyo, Tunakubaliana na kukiri kwamba wakristo wanapaswa kutumia maneno yao kwa hekima kwa kusema kweli na kwa kusema yale yanayoweza kuwajenga wengine. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba kwa kusema ili kuleta mema kwa wengine tunamhusisha Mungu ambaye pia hunena na kutimiza makusudi yake kwa neno lake.

Tunakana kwamba maneno ya wanadamu yana nguvu ya kuumba kama neno la Mungu. Tunakana kwamba wakristo wanaweza kuumba uhalisia kwa matamko ya unabii. Pia Tunakana kwamba kusema hali halisi kama ugonjwa au ukosefu wa kifedha kuna vuta au kuthibitisha hali hizo milele.

(Mithali 18:21; Mathayo 12:36-37; Waefeso 4:25-29; Wakolosai 4:6; Yakoko 1:19, 3:1-12)

Kifungu cha 10

Tunakubaliana na kukiri kwamba wanaume na wanawake wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Tunakubaliana na kukiri kwamba jambo hili linawapa thamani na kuwatenganisha kwa njia ya kipekee kutoka kwa viumbe vingine. Pia Tunakubaliana na kukiri kwamba kwa kuwa wameumbwa kwa mfano wa Mungu, wanadamu wanaweza kufanya kazi pamoja na Mungu kama viumbe vyenye akili kwa uumbaji wa kimwili kwa kuchukua mali ghafi na kubadilisha kuwa bidhaa yenye manufaa.

Tunakana kwamba kuumbwa kwa mfano wa Mungu kunawafanya wakristo kuwa “miungu midogo midogo” wenye mamlaka na uwezo wa kuumba vitu vyenye uhalisia kutoka kwa maneno yao. Tunakana kwamba maandiko yanapowaita viongozi na waamuzi :miungu” kwamba inamanisha wao ni viumbe vya viungu. Tunakana kwamba kuumbwa kwa mfano wa Mungu inamanisha kwamba Mungu alikuwa akijizalisha ndani yao kwa njia inayofanana na uzazi wa wanyama au wanadamu.

(Mwanzo 1:26-28, 2:19; Ayubu 38:1-42; Zaburi 82:6-7; Matendo ya Mitume 20:35; 2 Wathesalonike 3:10-12)

Kifungu cha 11

Tunakubaliana na kukiri kwamba imani ni zawadi itokayo kwa Mungu na ambayo hutufanya kuamini ahadi zake alizoziandika. Tunakubaliana na kukiri kwamba kwa wokovu imani ni lazima na ndiyo mkono wa pekee ambao tunapokea neema ya Mungu iokoayo. Tunakubaliana na kukiri kwamba pasipo na imani haiwezekani kumpendeza Mungu na kwa hivyo mkristo anapaswa kuishi katika imani maisha yake yote hadi mwisho. Pia Tunakubaliana na kukiri Mungu mara nyingi hufurahishwa wakati ambapo wanawe wanaomba ili waishi katika imani.

Tunakana kwamba imani ni nguvu ya mtu binafsi ambayo wakristo wanapaswa kutumia ili kuonyesha hali yoyote ambayo wanatamani. Tunakana kwamba imani ni wakala huru yenye nguvu ya kuumba na Mungu hulazimika kuheshimu. Pia Tunakana kwamba imani hutulinda kutokana na mateso.

(Waefeso 2:8-9; Wafilipi 1:29; 1 Petro 1:1; Waebrania 11:6,13)

Kifungu cha 12

Tunakubaliana na kukiri kwamba maisha ya akili na hisia ya mkristo ni muhimu sana kwa afya yake ya kiroho kwa ujumla. Tunakubaliana na kukiri kwamba jinsi mkristo hufikiri huathiri vilevile kuishi kwake. Kwa hiyo, Tunakubaliana na kukiri kwamba wakristo wana jukumu la kufanya akili yao kuwa mpya kwa kuendelea kutafakari kuhusu neno la Mungu.

Tunakana kwamba utawala wa picha akilini kunaleta nguvu ya uhalisia wa mambo hayo katika maisha ya mkristo. Tunakana kwamba mbinu za picha akilini ni mojawapo ya njia ambazo Mungu ameweka ili kuleta afya na utajiri.

(Warumi 12:1-2; Waefeso 4:17-24; Wafilipi 2:5-11; Wakolosai 3:12-17; 2 Petro 1:3)

Kifungu cha 13

Tunakubaliana na kukiri kwamba Mungu amechagua wazee wa kanisa kutumika kama wachungaji na waangalizi wa makusanyiko. Tunakubaliana na kukiri kwamba nafasi hii ni ya heshima ambayo pia ina wajibu mkuu. Tunakubaliana na kukiri kwamba kusudi la Mungu ni kwamba makusanyiko yakaweze kukua kiroho katika maisha yao hapa dunia kwa njia ya mafundisho na uangalizi wa uaminifu wa wachungaji. Kwa hiyo, Tunakubaliana na kukiri kwamba wazee wamepewa mamlaka ya kushauri makusanyiko yao kulingana na maandiko.

Tunakana kwamba mchungaji yeyote anaweza kushikilia hatima ya kiroho ya mkristo. Tunakana kwamba Mungu anaweza kumfunga mkristo yeyote kiroho kwa kutumia mchungaji na kwamba akaweze kwa imani yake kumtegemea huyo mtu. Zaidi ya hayo, Tunakana kwamba wakristo ni lazima wawe na heshima isiyo na mipaka kwa wachungaji wao la sivyo wapate laana kutoka kwa Mungu.

(Matendo ya Mitume 14:23, 20:28; Waefeso 4:7-12; Tito 1:5; Waebrania 13:17; 1 Petro 5:1-4)

Kifungu cha 14

Tunakubaliana na kukiri kwamba Mungu kama muumbaji ametangaza kusudi la kumuumba mwanadamu na mambo ambayo anapaswa kuyafuata, yaani kumtukuza Mungu na kumfurahia milele. Kwa hiyo tunakubaliana na kukiri kwamba mwanadamu huonyesha kukubaliana zaidi na kusudi la Mungu kwake wakati anapomthamini Mungu kuliko kitu kingine chochote alichokiumba. Wakati wa anguko, tamaa za mwanadamu ziliharibika na kutufanya tuwe na mwelekeo wa kuthamini zawadi nzuri anazotupatia Mungu badala ya kumthamini Mungu mpaji mwenyewe, uumbaji wake badala ya muumbaji mwenyewe.

Tunakana kwamba hukumu ya macho ya kimwili inaweza kufafanua kile kilicho chema bila kuzingatia ukweli wa Neno la Mungu. Tunakana kwamba kumshawishi mtu juu ya mambo mbalimbali yanayoongozwa na tamaa zake zilizoharibika ili kumpa motisha kunaweza kuzaa matunda yoyote mema. Tunakana kabisa kumtumia Mungu kama njia ya kujinufaisha kwa lolote, ikiwemo afya au utajiri.

(Mwanzo 1:1, 2:16-17; Kutoka 20:2-4; Isaya 43:6-7; Warumi 1:25; 1 Wakorintho 10:31; Waefeso 2:1-10)

Waliotia Sahihi Mwanzoni

Allan Waruhiu

Mchungaji , Mercy Nairobi Church, Kenya

Arphaxad Chege

Mchungaji, Presbyterian Church of East Africa, Kenya

Benard Kariuki Mbugua

Mchungaji, GracePoint Church Thika Road, Kenya

Bernard Kuria

Mchungaji, Trinity Baptist Church Kasarani, Kenya

Charles Maina Njau

Mchungaji, Buruburu Baptist Church, Kenya

Chopo Mwanza

Mchungaji, Faith Baptist Church Riverside, Zambia

Chris Kiagiri

Mchungaji, North Point Baptist Church, Kenya

Confex Makhalira

Mchungaji, Christ Presbyterian Church, Malawi

Dan Gachuki

Mchungaji, Emmanuel Baptist Church, Kenya

Daniel Mutuku

Mzee wa Kanisa, Buruburu Baptist Church, Kenya

Danson Ottawa

Mkurugenzi Mkuu, Africa Centre for Apologetics Research (ACFAR), Kenya

Dieudonné Tamfu

Mchungaji, Église Baptiste Bethléem, Yaoundé, Cameroon

Dominic Kabaria

Mchungaji, Trinity Baptist Church, Kenya

Emmanuel Kwasi Amoafo

Kasisi, Anglican Church of Kenya, Kenya

Fidel Nyikuri

Mchungaji, GracePoint Church Limuru, Kenya

Graham Heslop

Mhariri Mkuu, TGC Africa, South Africa

Harrison Mungai

Mchungaji, GracePoint Church Kikuyu, Kenya

Isaiah Maina

Mchungaji, Trinity Baptist Church Kasarani, Kenya

Joe Mwita Thwagi

Mchungaji, Upendo Gospel Community Church, Kenya

John Musyimi

Mchungaji, North Point Baptist Church, Kenya

Joseph Masunga

Mchungaji, Injili Bible Church, Kenya

Joshua Lemayian

Mchungaji, Emmanuel Baptist Church, Kenya

Ken Mbugua

Mchungaji, Emmanuel Baptist Church, Kenya

Kevin Nyagaka

Mchungaji, Upendo Gospel Community Church, Kenya

Kyle Tamblyn

Mchungaji, Honeyridge Baptist Church, South Africa

Mark Ben Thuku

Mchungaji Mratibu, North Point Baptist Church, Kenya

Matt Elmore

Mkurugenzi, Kuza, Kenya

Mpumelelo Kunene

Mchungaji, Heritage Baptist Church, South Africa

Peter Kamau

Mchungaji, GracePoint Church Waiyaki Way, Kenya

Philip Ipala

Mchungaji, Cornerstone Baptist Church, Nairobi, Kenya

Philip S. Hunt

Mchungaji, Kitwe Church, Zambia

Raymond Ndung'u

Mwalimu Msaidizi, Nairobi Institute of Reformed Theology, Kenya

Rodgers Atwebembeire

Mkurugenzi wa Kikanda, Eastern Africa, Africa Centre for Apologetics Research (ACFAR), Uganda

Samuel O. Oluoch

Mchungaji, Grace Baptist Church, Nairobi, Kenya

Selian Meoki

Mkurugenzi Mtendaji, Ekklesia Afrika, Kenya

Seth Diang'a

Mchungaji, Redeemer Bible Church, Kenya

Titus Mburu

Mzee wa Kanisa, GracePoint Church Kikuyu, Kenya

Tommie van der Walt
Mkurugenzi Mtendaji wa Imprint; Mzee wa Kanisa, Brackenhurst Baptist Church, South Africa

Jinsi Unavyoweza Kushiriki

1. Weka sahihi kwa kauli kwenye tovuti
www.africastatement.org/sign

2.Unaweza kushiriki toleo la taarifa mtandaoni kwa wengine kwenye mit andao ya kijamii : **www.africastatement.org**

3. Waelekeze wengine kwenye rasilimali sahihi kuhusu injili ya ufanisi, kama zile zilizoonyeshwa chini ya
Marejeo yanayopendekezwa

4. Fikiria kutumia tamko hili kuchunguza washirika watarajiwa kwa kanisa lako, seminari, au huduma ya Kanisa**.**

Marejeo yanayopendekezwa

John Musyimi
Injili Feki: Kutambua Umaskini wa Injili ya Ufanisi
Nairobi: Ekklesia Afrika, 2019
www.ekklesiaafrika.org
Ken Mbugua et al.
Ufanisi? Tafuta Injili ya Kweli
Nairobi: ACTS/TGC, 2015
www.actskenya.org

Emmanuel Kwasi Amoafo

Simama kwa Ajili ya Injili: Kuurejesha Kanisa Kwenye Mkondo Sahihi

Oasis International, 2022
www.oasisinternationalpublishing.com